

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA YAPATA
MWENYEKITI NA MAKAMISHNA WAPYA.**

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1. Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma imepata Mwenyekiti na Makamishna wapya watakaioiongoza Tume katika kipindi cha miaka mitatu baada ya Mwenyekiti na Makamishna wa zamani kumaliza kipindi chao Januari 7, 2007.
2. Kwa mamlaka aliyopewa kikatiba pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kifungu 9(1) Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamishna 5 wa Tume ya Utumishi wa Umma tarehe 1 Agosti, 2007 na kuwaapisha tarehe 14 Agosti, 2007, Ikulu Jijini Dar es salaam.
3. Kufuatia uteuzi huo, aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti ni Bw. Jovin Barnabas Kitambi. Aidha walioteuliwa kuwa Makamishna ni Edris Ramadhan Mavura, David Salum Mfangavo, Cecilia Simon Shirima, Mary Ndekarishwa Seth Mzeru na Dkt. Gabriel Leonard Upunda.
4. Mwenyekiti aliyemaliza kipindi chake ni Mhe. Jaji (Mstaafu) Lameck Mfalila. Kuhusu Makamishna waliomaliza kipindi chao ni Balozi Norman Kiondo, Bibi Nderikyo Ligate, Bibi Monica Mbapila, Bw. Leonard Msaki, Bw. Ashour Abbas na Bw. Kenya Hassan.
5. Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi Na.8 ya mwaka 2002 na kuanza rasmi kazi zake Januari 7, 2004 inaye Katibu ambaye ndiye Mtendaji Mkuu na Afisa Mhasibu, Bibi Thecla W. Shangali.
6. Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake Tume inazo Idara 5 zinazosimamiwa na Manaibu Katibu. Idara hizo ni Idara ya Utumishi wa Walimu, Utumishi wa Afya, Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji, Utumishi wa Serikali za Mitaa na Idara ya Utumishi Serikalini. Tume inazo pia Ofisi Mikoani na Wilayani Tanzania Bara.

Ndugu Msomaji, iwapo una maoni, ushauri au maswali tuandikie:

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.